# 1 FOR 50 Mafunzo ya Hatua Zinazofuata

## Kujenga Familia Imara katika Ulimwengu wa Leo

## Mwongozo wa Mwalimu wa Familia na Ulezi Somo la 2

### Malengo

- Kutambua na kufahamu mazingira ambayo familia zetu zinaishi na masuala yanayowakabili
- Kutathmini sifa zinazofanya familia kuwa na nguvu
- Kuombea familia zewe na nguvu

### MAELEZO YA SOMO

Somo hili linawaruhusu washiriki kuangalia familia katika maeneo yao ya karibu na kujadili baadhi ya masuala ambayo familia hizi hukabiliana nayo. Washiriki wanagundua sifa za familia yenye nguvu kwa kuangalia mfano wa Mordekai na Esta.

### MUHTASARI WA SOMO

| | |
|---|---|
| • Kujitayarisha: Machafuko | 10 |
| • Familia katika Maeneo Yetu | 20 |
| • Masuala Yanayozikabili Familia zetu Leo | 30 |
| • Sifa za Familia Imara | 15 |
| • Kumaliza | 5 |
| Takriban Jumla ya Dakika | **80** |

### MAELEZO YA JUMLA YA MAANDALIZI

- Andaa moyo wako/omba
- Soma somo lote kabla ya wakati
- Fanya marekebisho inavyohitajika kwa mpangilio wako
- Kusanya nyenzo/vifaa unavyohitaji

### Maandiko yatakayotumika katika somo hili:

- Esta 2:5-11; 3:8-11; 4:1-5, 12-17; 8:1-2; 10:3

### Nyenzo/vifaa zinazohitajika kwa somo hili:

- Biblia
- Vidokezo vya Mshiriki
- Ubao mweupe au chati mgeuzo na vyombo vya kuandikia
- Vitu laini 3-4 kwa kila watu 10-15 (soksi, mifuko ya maharagwe, na zinginezo.)
- Karatasi tupu (karatasi 1 kwa kila kikundi)
- Hiari: Kadi za Familia na Mapato
- Hiari: Kadi Imara za Chati ya Pai ya Familia

Video:

- Maisha Kati ya Masikini na Tajiri

## KUJITAYARISHA

Dakika 10

**Machafuko**

**Vifaa Vinavyohitajika:** vitu vidogo vidogo vitatu au vinne kama vile soksi zilizokunjwa, mifuko ya maharagwe, mipira kwa kila kikundi cha watu 10-15.

(Waambie washiriki waunde miduara ya washiriki 10-15. Zunguka kwenye duara na kila mshiriki ajitambulishe kwa jina. Mpe mshiriki kitu kimoja. Waagize kumwita mtu mwingine kwenye duara, "Pokea, _____ (jina la mtu)!" na kisha kumtupia mtu huyo kitu. Mtu anayekamata kitu kisha anasema, "Asante, _____ (jina la mrushaji)!" na kisha kurudia kile mtu wa kwanza alifanya, akisema, "Pokea_____!" na kisha kuitupa kwa mtu mpya. Majina lazima yasemwe kila wakati kitu kinapotupwa au kunaswa. Hakuna mpangilio uliowekwa wa kutupa kitu. Baada ya kikundi kuwa sawa na kitu kimoja, tambulisha cha pili, kisha cha tatu na cha nne. Itazidi kuwa mchafuko unapoongeza vitu zaidi vya kurusha.)

Baada ya mchezo kumalizika, jibu maswali yafuatayo:

- **Ni nini kilikuwa changamoto katika mchezo huo?**
- **Ni nini kilikusaidia kuendelea kuwa makini na kufanikiwa?**
- **Mchezo huu unatukumbusha nini kuhusu familia katika ulimwengu wa leo?**

**Chaguo la Video: Maisha Kati ya Maskini na Tajiri**
https://www.youtube.com/watch?v=rxKqBEqb8fY

Kila familia hukumbana na changamoto inapopitia ulimwengu wa leo wenye machafuko. Katika somo hili tutaangalia familia leo, baadhi ya masuala yanayowakabili, na jinsi familia zinavyoweza kuwa imara licha ya changamoto zinazowakabili.

## FAMILIA KATIKA JAMII YETU

Dakika 20

> Mpango mkuu wa Mungu wa kukua watu wenye afya katika jumuiya na makanisa ni familia. Lakini ulimwenguni kote tunaona familia zikihangaika, zikivunjika, na kufadhaika. Wacha tutumie wakati huu kutazama familia hapa katika jamii hii.


SOMO LA 2
KUJENGA FAMILIA IMARA KATIKA ULIMWENGU WA LEO

Familia katika Maeneo Yetu

Je, ni miundo ipi ya familia tunaiona katika utamaduni wetu leo?

Masuala Yanayozikabili Familia Zetu Leo

Maisha ya kila siku yakoje? Nè masuala gani ya kiritendo yapo kabisa kwenye familia?

Nitoa ikoje? Je, kuna shida?

Changamoto ya kuiwa ni ipi?

Je, kuna masuala kati ya ndugu? Kama gani?

Masuala yao ya kifedha ni yepi?

Je, ni masuala gani mengine ya kijamii yanayoathiri familia?

| Masuala/Shida Zinazozikabili Familia Zetu Leo | Nguvu tunazoona katika Familia |
|---|---|
| | |

Sifa za Familia Imara

FAMILIA NA ULEZI
UKURASA WA 1

(Wagawe washiriki katika vikundi vya watu watatu au wanne. Wape kila kikundi karatasi. Wakumbushe kuhusu miundo ya familia iliyojadiliwa katika somo la 1 na eleza kwamba sasa wataangalia **miundo ya familia katika utamaduni wetu leo kwa kuchora mifano ya makundi mbalimbali ya familia wanayoyaona.** Wanaweza kuchora hataka na kwa urahisi kutumia vijiti,wanapaswa kuchora wanaume, wanawake na watoto. Kundi la familia lingewakilisha watu wote wanaoishi katika nyumba moja. Kabla ya vikundi kuanza, itasaidia kuchora mifano michache kwenye ubao kama vile familia ya wazazi wawili yenye watoto, mzazi mmoja mwenye watoto, wazazi wawili wasio na watoto, vizazi vitatu vinavyoishi pamoja,... Wakumbushe washiriki kuwa familia ya kikundi ya mzazi mmoja anaweza kuwa na sababu nyingi kama vile talaka, kifo, mama ambaye hajaolewa, na zinginevyo)

Baada ya dakika tano vikundi vishiriki "familia" mbalimbali walizozitambua. Kila kikundi kipya kinaposhirikiwa, chora kwenye ubao mweupe na uweke jina hadi makundi yote ya familia yatakapo wakilishwa.)

Kama vile tulivyoona katika Maandiko, tunaona pia kwamba kuna picha nyingi tofauti za "familia" katika utamaduni wetu. Tunapofikiria jinsi ya kuhudumia familia, lazima tukumbuke kwamba hakuna picha moja ya jinsi “familia” inavyoonekana. Huenda huduma yetu pamoja na familia ikahitaji kubadilika-badilika kwa sababu ya tofauti hizo nyingi.

Sasa tutaangalia kwa undani zaidi baadhi ya familia mahususi katika maeneo yetu na changamoto zinazowakabili.

## MASUALA YANAYOKABILI FAMILIA ZETU LEO

Dakika 30

(Eleza kwamba familia katika maeneo yetu jirani zina mienendo tofauti na viwango tofauti vya kiuchumi. Tengeneza vikundi vya watu watano au sita. Wape kila kikundi, kikundi kimoja cha familia kwenye ubao, kila kikundi kiwe na kikundi tofauti cha familia. Au, unaweza sambaza Kadi ya Familia ya hiari kwa kila kikundi. Pia kipe kila kikundi kiwango cha mapato: maskini, wastani au tajiri. Kazi ya kila kikundi ni kuunda hali ya familia kwa kutumia kambi ya familia na hali ya kiuchumi waliyopewa. Kikundi kitaamua umri na jinsia za watoto, kazi za wazazi, huunda sababu ya familia kuwa katika hali hii, na kuamua ikiwa familia ni ya Kikristo au isiyo ya Kikristo.

Wape vikundi dakika kumi kufikiria na kujadili jinsi maisha yanavyoweza kuwa kwa familia yao ya uwongo, kwa kutumia maswali yaliyo kwenye maelezo ya washiriki kama mwongozo. Himiza vikundi kuwa wabunifu!

- **Maisha ya kila siku yakoje? Ni masuala gani ya kivitendo yanaiharibu familia?**
- **Ndoa ikoje? Je, kuna masuala?**
- **Je, ni masuala gani ya uzazi?**
- **Je, kuna masuala ya ndugu? Kama gani?**
- **Masuala yao ya kifedha ni yapi?**
- **Je, ni masuala gani mengine ya jamii yanayoathiri familia?**

Iwapo kuna vikundi vichache tu, ruhusu kila kikundi kieleze kwa ufupi familia yao kwa washiriki wengine na kubadilishana mawazo kuhusu aina ya masuala ambayo familia yao inahusika nayo zaidi. Ikiwa kuna vikundi kadhaa, acha vikundi vishiriki kuhusu familia zao na kikundi kingine.)

**Je, familia hizi zinafananaje na familia halisi katika maeneo yako?**

(Waombe washiriki kuchukua dakika tano katika vikundi vyao kujadili maswali mawili yafuatayo:

- **Je, ni masuala/mahitaji gani makubwa yanayokabili familia za wenyeji katika utamaduni wetu?**
- **Je, ni nguvu gani tunazoziona katika familia za utamaduni wetu?**

Shiriki majibu na kundi kubwa, ukiandika mawazo muhimu ubaoni. Tafakarini pamoja juu ya uchunguzi wao.)

Inaweza kuwa rahisi kuzingatia tu matatizo yanayokabili familia zetu leo, lakini pia tunahitaji kutambua na kusherehekea nguvu tunazoziona katika familia. Ingawa baadhi ya familia zina changamoto na matatizo, bado wanaweza kuwa na nguvu. Sasa tutaangalia sifa za familia zenye nguvu, tukianza na mfano wa kibiblia: Esta na mjomba wake, Mordekai.

## SIFA ZA FAMILIA IMARA

Dakika 15

**Mordekai na Esta** hawakuwa familia ya kitamaduni: msichana yatima ambaye alilelewa na mjomba wake. Hata hivyo, **tunapoitazama familia hii kwa karibu zaidi**, tutawaona wakionyesha sifa nyingi za familia yenye nguvu. Katika vikundi vya watu wawili au watatu, soma vifungu vifuatavyo katika kitabu cha **Esta: 2:5-11; 3:8-11; 4:1-17; 8:1-2; 10:3. Tambua sifa za familia yenye nguvu ambazo unaona.**


Vidokezo vya Mshiriki
SOMO LA 2 KUJENGA FAMILIA IMARA KATIKA ULIMWENGU WA LEO

Soma Esta 2:5-11; 3:8-11; 4:1-5, 12-17; 8:1-2; 10:3. Angalia kwa makini familia ya Mordekai na Esta. Tambua sifa za familia yenye nguvu ambazo unaona.



Je! ni nini kinachotokea kwa familia ikiwa moja au zaidi ya sifa hizi haipo?

Ja, ni matatizo ngapi ambayo hukabili familia za leo yanatokana na kutokuwepo kwa moja au zaidi ya sifa hizi?

Tafakari juu ya familia yako, au familia uliyoishiwa, kwa kuangalia sifa sita za familia zenye nguvu.
Ni sifa gani zilikuwepo?

Ni sifa gani hazikuwepo?

Ni sifa gani ambazo huenda Mungu anakuhimiza ustawishe?

FAMILIA NA ULEZI
UKURASA WA 2

> Ingawa Mordekai na Esta hawakuwa familia ya kitamaduni, tunaona sifa sita kuu za familia yenye nguvu katika simulizi la Biblia tunalosoma. Tutawawakilisha kama vipande vya keki iliyokatwa.

(Ama chora chati ya mviringo ubaoni na uongeze sifa unapozijadili au onyesha Kadi za Chati ya sehemu moja ya keki baada ya nyingine. Kwa kila ubora, ielezee na kisha waalike washiriki kueleza jinsi walivyoona ubora huu katika kitabu cha Esta. )

KUWA NA UWEZO WA KUBADILI
Wana uwezo wa kushughulikia shida na kutatua shida
(Mordekai alibadili utaratibu wake, mwonekano, na cheo chake ili kuombea na kuomboleza ku

KUJITOA
Wamejitolea kusaidiana, kusaidiana na kutunzana
(Mordekai alimlea binamu yake yatima, akakaa karibu naye)

KIROHO
Wana ahadi ya kiroho
(Mordekai alizungumza kwa ajili ya ustawi wa watu wa Mungu)




MUDA
Wanatumia muda pamoja
(Kila siku Mordekai aliingia kwa Esta)

KUTHAMINI
Wanaonyesha shukrani/heshima kwa kila mmoja wao
(Mordekai akafanya kama Esta alivyoagizwa, Esta akafanya kama Mordekai alivyoomba na wote wawili wakaheshimiwa)

MAWASILIANO
Wana mawasiliano mazuri ya kifamilia, wanazungumza wao kwa wao
(Mordekai alimkataza Esta kufichua historia ya familia yake)

Jadili maswali yafuatayo kama kikundi kwa ujumla:

- **Je! ni nini kinachotokea kwa familia ikiwa moja au zaidi ya sifa hizi hazipo?**
- Turudu nyuma kidogo fikiria orodha ya masuala/mahitaji ya familia tuliozungumzia mapema katika somo hili, **ni matatizo mangapi ambayo familia za leo zinazokabili nazo na yanatokana na kutokuwepo kwa moja au zaidi ya sifa hizi?**

(Sehemu hii si lazima lakini ikiwa una wakati: Tumia sifa sita za familia yenye nguvu katika hali halisi ifuatayo: Fikiri kwamba mtoto wako, mwenye umri wa miaka 12, amechelewa kurudi nyumbani kwa saa mbili. Suruali yake mpya imechanika na ana jicho jeusi kutokana na kushiriki vita na wenzake. Gawa katika vikundi sita na uwape kila kikundi sifa moja kati ya sita za familia yenye nguvu.Vikundi lazima vijadili jinsi sifa hiyo inaweza kuonyeshwa na wazazi/familia ilio katika hali hiyo.Baada ya dakika chache vikundi vinaweza kufanya mchezo wa kuigiza kama drama au ripoti kwa kundi zima.)

Ni muhimu kujua sifa zinazofanya familia kuwa na nguvu. Lakini acheni tutumie somo hili kwa familia zetu wenyewe. Familia yako ina nguvu kiasi gani?

## KUMALIZA

dakika 5

(Waruhusu washiriki kutafakari juu ya familia zao wenyewe, au familia ambako walilelewa, kwa kuangalia sifa sita za familia zenye nguvu.

- **Ni sifa gani zilikuwepo?**
- **Ni sifa gani hazikuwepo?**
- **Ni sifa gani ambazo huenda Mungu anakuhimiza ustawishe?**

Kuwa na muda wa kutafakari kwa utulivu ili kuruhusu watu kuandika majibu yao.

Maliza kwa kuwaongoza washiriki kuomba kwa njia tatu zifuatazo:

- Mshukuru Mungu kwa ajili ya familia imara na sifa nzuri unazoona katika familia na familia yako mwenyewe.
- Omba kwa ajili ya ulinzi juu ya familia.
- Mwombe Mungu aingilie kati masuala ya familia yaliyotambuliwa wakati wa somo.)